

Ni Muhimu Kumwamini Mungu!

Na
Rod Rutherford

Tunaishi katika ulimwengu wa watu wasioamini. Watu wengi wamemkubali Shetani na hawana imani kwamba Mungu ni muumbaji wa dunia hii. Wanasayansi wanampinga Mungu kuwa muumbaji wa dunia hii. Sababu za kumpinga Mungu kuwa muumbaji hazina maana yo yote ile.

Imani ya kwamba Mungu ni muumbaji hiyo ni muhimu sana kwa sababu uumbaji unahitaji muumbaji, kama mtu ataona nyumba nzuri hana budi kujiuliza maswali, hii nyumba nzuri imetoka wapi? Atatambua kwamba nyumba hiyo imejengwa. Hii ni sawa kabisa na dunia yetu hii, kuna mtu ambaye aliumba, kila nyumba hujengwa na mjenzi fulani, Mungu ndiye mjenzi wa vitu vyote, Ebr. 3:4.

Imani ya kwamba Mungu ni muumbaji wa vitu vyote, hiyo ni imani nzuri kwa sababu uzima huja kutoka kwa uzima na inabidi tuelewe kwamba kitu kilichokufa hakiwezi kuzaa kitu hai. Zamani huko ulaya watu wengi waliamini kwamba vitu ambavyo havina uhai vinaweza vikazaa vitu hai. Louis Pasteur Mwanasayansi Mkuu wa Ufaransa katika karne ya kumi na tisa alisema imani hiyo ni potovu, akasema uzima utatoa uzima.

Hebu fikiriri, Je! Kiota cha ndege kinaweza kumtengeneza ndege au kumuumba? Je, gari linaweza kumfanya mtu aliendeshe? Au ni mtu ndiye anayeweza kulitengeneza na kuliendesha?

Hakuna sababu kuwa vitu vyote duniani vilivyopo vimetokana na vitu visivyo na uhai bali vitu vyote vilivyopo vimeletwa na kuwekwa na Mungu wanyama pia mimea.

Vile vile ni muhimu kuamini kwamba Mungu ndiye muumbaji kwa sababu ya mpango na makusudi kuleta kanuni mbali mbali za manufaa. Jua lina umbali wa 93,000,000 maili.

Kutoka dunia ni, kama jua lingekuwa karibu dunia ingechomwa na jua hata kuteketea, na kama ingekuwa mbali zaidi dunia ingeganda.

Je! Haya yalitokea kwa bahati tu, au ulikuwa ni mpango wa Mungu.

Ni busara kuamini hapo mwanzo Mungu aliumba Mbingu na nchi, Mwa. 1:1. Wajinga wanasema mioyoni mwao kwamba hakuna Mungu, Zab. 14:1.

www.kanisalakristo.com

